JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS (TAMISEMI)
HALMASHAURI YA LUSHOTO
Magambasec2007@gmail. Com. 0717053340 /0621980975

SHULE YA SEKONDARI MAGAMBA.
S.L. P 99,
LUSHOTO.

KUMB.KUMB. Na MGSS/JI/Fv/2022/23.
YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO

CHA TANO JUNE 2022.

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa

kujiunga kidato cha tano mwaka 2022

katika shule ya Sekondari Magamba.

Magamba sekondari ni shule ya kutwa ya wavulana na wasichana kwa kidato cha kwanza mpaka cha nne, na bweni kwa kidato cha tano na sita wavulana kwa tahasusi za PCM na PCB.

Shule ya sekondari Magamba ipo Wilaya ya **Lushoto** Tarafa ya Lushoto Mkoa wa**Tanga**. Shule iko takriban kilomita 13 kutoka makao mkuu ya wilaya.Ukiwa Lushoto mjini unapanda magari ktk kituo cha Magamba kilichopo karibu na benki ya NMB tawi la Lushoto kwa nauli ya shilingi elfu moja mpaka elfu moja na mia tano kwa usafiri wa basi/noa. Ukiwa umepanda mabasi yaendayo Mlalo /Mtae kutoka Dar/Arusha/Tanga n.k ushuke Magamba sekondari . Umechaguliwa kutokana na kufaulu vizuri mtihani wako wa kidato cha nne. Hivyo ukiwa Magamba unatakiwa kusoma kwa bidii na maarifa, ili utumie nafasi uliyopewa na serikali vizuri kwa manufaa yako, ya jamii na serikali. Ukiwa Magamba Sekondari utalazimika pia kufuata sheria, kanuni, taratibu na maadili ya uanafunzi, (sheria za shule zimeambatanishwa) .

Utaripoti shuleni tarehe 13/06**/2022** bila kuchelewa ukiwa tayari kwa kuanza masomo. Utajaza kiambatanisho A na B na ufike navyo shuleni siku ya kuripoti. Fika na nakala ya cheti cha KUZALIWA na nakala ya results slip ya matokeo yako ya kidato cha nne .

MAHITAJI MUHIMU YA SHULE

Kila mwanafunzi ajishonee mwenyewe sare zifuatazo:

1.1 SARE YA SHULE.

1	Suruali mbili (2)rangi yake ni blue bahari.
2	Shati nyeupe jozi mbili (2) za mikono mirefu (tetron).
3	Socks nyeusi kuanzia jozi mbili.
4	Nguo za michezo.
5	Masweta mawili ya rangi ya kijivu kwa kila mwanafunzi
6	Viatu vyeusi vya ngozi. Visiwe buti au vyenye visigino VIREFU.VIWE VYA KAMBA.

MAHITAJI MENGINE.

(a) Raba za michezo
(b) Vifaa vya chakula ikiwa ni pamoja na sahani na kijiko,kikombe na bakuli.
(c) Vifaa vya usafi vikiwa ni ndoo ndogo moja, fagio, jembe na panga. Mopper, hard broom.

2. VIFAA VYA DARASANI

(a) Afike na daftari za kutosha kwa masomo yake atakayosoma, kalamu za kutosha. SCIENTIFIC calculator na mathematical set.
(b)faili lake binafsi la kutunzia kumbukumbu zake za majaribio na mitihani.
(c) Dictionary.

Ada na michango mingine.

1.Ada ni 70,000/=kwa mwaka. Unaweza kulipa 35,000/=kwa temu.
2.Taaluma ni 15,000/= kwa muhula.
3.Tahadhari ni ni 20,000/=ambayo hairudishwi.
4.Kitambulisho ni 6,000/=
5.Mchango wa ujenzi na ukarabati ni 20,000/=
6.mpishi na mlinzi ni 20,000/=kwa muhula.
7.Rimu 1(karatasi za mitihani A4 (plain) raser au hp.
8.Bima ya afya, au fedha kwa ajili ya matibabu.
9.Godoro futi 2.5 kwa 6.(dodoma au confy)
10.Shuka mbili (pink) na blanket na nguo nzito za kuzuia baridi.
11.Picha (passport size) nne.

Fedha zote ziwekwe kwenye akaunti namba 41603100008,(Magamba secondary school fund account).

Utapokelewa iwapo utakuwa umelipa michango hiyo na kukabidhi bank paying slip kwa Mhasibu wa shule.

Karibu sana Shule ya Sekondari Magamba.

_____

PETER MICHAEL NYELLO.

Mkuu wa shule.

KIAMBATISHO A
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI MAGAMBA S.L.P 99,LUSHOTO.
SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

1. **HESHIMA**

(a) Mwanafunzi atasimama kumsalimia mwalimu au mtu yoyote aliyemzidi umri anapopita anapoingia darasani au hata akiwa nje ya darasa .
(b) Mwanafunzi atatumia lugha safi (inayokubalika) wakati wote kati yake na wenzake na kwa watu wengine akiwa shuleni au nje ya shule.
(c) Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote.
(d) Mwanafunzi ataitika wito maramoja na kumfuata mwalimu anayemuita katika mazingira ya shule.
(e) Mwanafunzi anapaswa kuheshimu kazi yoyote anayopewa na mwalimu au mlezi wake.
(f) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa na picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na alama zingine za Taifa.
(g) Mwanafunzi atasimama katika mstari wakati wote anaposubiri kupata huduma.
(h) Mwanafunzi atakaa kimya wakati wote akiwa darasani, asitoke nje ya darasa au eneo la shule bila ruhusa ya mwalimu.

2. MAHUDHURIO

(a) Mwanafunzi anatakiwa ahudhurie vipindi vyote vya darasani kwa muda wote wa masomo. Atatakiwa kufika shuleni kwa tarehe zote zilizopangwa na anapokosa kufika siku anapofika akatoe taarifa kwa mmojawapo wa hawa:
   i. Mwalimu wa zamu wa siku hiyo
   ii. Mwalimu wa darasa.
   iii. Makamu wa mkuu wa shule.

(b) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano ya shule kama vile mabaraza ya shule, ukaguzi wa usafi na kupandisha bendera ya Taifa.
(c) Mwanafunzi atatakiwa kufanya shughuli zote shuleni kama zilivyopangwa kwenye ratiba ya shule na pia anatakiwa kuwahi anapotakiwa au anaposikia kengele.
(d) Mwanafunzi anatakiwa kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote anayopewa na mwalimu wa somo darasani. Akikosa jaribio au mtihani wowote akamuone mwalimu wa somo na mwandamizi taaluma.

3. SARE YA SHULE NA USAFI

Mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare safi ya shule wakati wote wa saa za shule. Atakuwa na vazi tofauti pale tu atakapo agizwa kama vile nguo za michezo wakati wa michezo au nguo za kazi. Sare ya shule iwe safi muda wote.

4. MAKATAZO

4.1 SEHEMU ASIZORUHUSIWA KUTEMBELEA MWANAFUNZI

(a) Mwanafunzi asitembee sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali au ruhusa:
   i. Ofisi ya walimu
   ii. Maabara
   iii. Nyumba za walimu au wafanyakazi wa shule. Majengo yasiyotumika. Na eneo la mabwawa ya samaki.
(b) Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutembea sehemu hizi:
   i. Vilabu vya pombe
   ii. Kumbi za starehe
   iii. Nyumba za kufikia wageni
(c) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa/kibali cha mwalimu.

4.2 NI MARUFUKU

(a) Kuiba mali ya mtu binafsi au umma
(b) Kufanya uasherati, ubakaji, usagaji au ushoga
(c) Kulewa kilevi cha aina yeyote au kuvuta sigara au bangi
(d) Kupiga au kupigana
(e) Kuharibu mali ya umma
(f) Kuoa au kuolewa
(g) Si ruhusa kwa wanafunzi kumiliki au kuwa na simu kamera, radio au shuleni. Iwapo mwanafunzi atapatikana na vitu hivyo hapa shuleni vitachukuliwa na havitarudishwa kamwe na mwanafunzi atalazimika kufukuzwa shule endapo atapatikana na vitu hivyo. Ili kuepuka adha hiyo hakikisha kuwa humpi mwanao vitu hivyo visivyokubalika shuleni. Ili kurahisisha mawasiliano, unaweza kumwandikia mwanao namba ya simu ambayo utaitumia akihitaji mawasiliano na mzazi au mlezi na atasaidiwa mawasiliano ya simu na ofisi ya mkuu wa shule kupitia namba zilizoorodheshwa hapo juu.

5. MAKOSA YANAYOMFUKUZISHA SHULE

(a) Uasherati, ubakaji, usagaji,ushoga, kuoa au kuolewa.
(b) Wizi ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
(c) Kuvuta bangi.
(d) Kupiga au kupigana
(e) Kudharau bendera ya taifa na kuharibu mali ya umma.
(f) Kupata, kutoa mimba au kusababisha mimba shuleni au nje ya shule.
(g) Kugoma, kuongoza, kuchochea mgomo au vurugu, kuvuruga amani au usalama wa watu.
(h) Kukashifu na kukataa adhabu halali
(i) Kutumia au kumiliki simu shuleni.

ANGALIZO

Ni jukumu la mwanafunzi kufuata sheria na taratibu zilizowekwa ili kuepuka adhabu na kufukuzwa shule. Walimu shuleni ni waelekezaji, walezi, waelimishaji na washauri. Mwanafunzi akiwasikiliza atafika kule anakotarajia, alikopanga. Aidha, shule ina utaratibu wa kumuita mzazi/mlezi shuleni pale ambapo mwanafunzi amepatikana na utovu wa nidhamu mkubwa hivyo ni vizuri kuwaasa Watoto kuzikatia sheria na taratibu za shule ili kuepuka usumbufu wa kuitwa shuleni.

Jina ……..saini…….tarehe…….

KIAMBATISHO B.

THE UNITED REPBRIC OF TANZANIA
PO-REGINAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

MAGAMBA SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 99,

LUSHOTO .

TO MEDICAL OFFICER.
……
…….
……

REF: STUDENT MEDICAL EXAMINATION FORM

Please Examine student named ……in respect of these areas and any other areas(S) deemed relevant in connection to whether the student has problems related to

(a) Sight Yes/No. If yes, state……..

……

(b). Hearing Yes/No If yes, state……
……

(c). T.B. or any other chronic Diseases. Yes/No If yes, state…….
……
……

(d) Blood pressure. Yes/No If yes, state……
……
(e) Any physical impairment(s). Yes/No If yes, state……
……

Do you therefore recommend this pupil to pursuer studies at this school?.
……
……
……
…….

Name…… signature……date……..
Official title…… Official stamp